JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

# Mwongozo kuhusu Muswada Binafsi wa Sheria

Machi, 2018

PARLIAMENT O
BUNGE LA T
UHURU NA

# Mwongozo kuhusu Muswada Binafsi wa Sheria

# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| **1.0 UTANGULIZI** | **1** |
| **2.0 MAANA YA MUSWADA WA SHERIA** | **2** |
| **3.0 AINA ZA MISWADA YA SHERIA** | **3** |
| (a) Muswada wa sheria wa Serikali | 3 |
| (b) Muswada Binafsi wa Sheria | 3 |
| **4.0 UTARATIBU KUHUSU MUSWADA BINAFSI YA SHERIA** | **4** |
| **5.0 MAANDALIZI YA MUSWADA BINAFSI** | **5** |
| **6.0 SHERIA ZINAZOPASWA KUFUATWA KATIKA MCHAKATO WA KUTUNGA SHERIA** | **6** |
| (a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Mwaka 1977 | 6 |
| (b) Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1964 | 6 |
| (c) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 | 7 |
| (d) Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 | 7 |
| (e) Sheria ya Mapitio ya Sheria, Sura ya 4 | 7 |

(f) Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 8

**7.0 MASHARTI YA JUMLA YA MUSWADA BINAFSI WA SHERIA 9**

(a) Kuandika Muswada Binafsi wa Sheria 9

(b) Kuandaa Taarifa ya Kuandaa Muswada Binafsi wa Sheria 10

(c) Muswada Kutangazwa katika Gazeti la Serikali 10

(d) Muswada Binafsi wa Sheria wa Dharura 11

**8.0 MAENEO AMBAYO MBUNGE HATAWEZA KUPENDEKEZA MUSWADA BINAFSI WA SHERIA 13**

**9.0 NAFASI YA SEKRETARIETI YA BUNGE KATIKA UANDAAJI WA MUSWADA BINAFSI YA SHERIA 15**

**10. HATUA ZA MUSWADA KUWASILISHWA BUNGENI 16**

(a) Muswada Kusomwa Mara ya Kwanza 16

(b) Muswada kupelekwa kwenye Kamati 17
(c) Muswada Kusomwa Mara ya Pili 18
(d) Muswada Kufanyiwa Kazi na Kamati ya Bunge Zima 21
(e) Muswada Kusomwa Mara ya Tatu 23

**11. MUSWADA KUPATA RIDHAA YA RAIS 24**

**12. KUANZA KUTUMIKA KWA SHERIA 25**

**13. MATARAJIO KUTOKANA NA MWONGOZO HUU 25**

**14. HITIMISHO 26**

## 1.0 UTANGULIZI

Madaraka ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kutunga Sheria yamewekwa kwa mujibu wa Ibara ya 63 na Ibara ya 64 zikisomwa pamoja na Ibara ya 97 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara ambayo katika Mwongozo huu itarejewa kama Katiba. Madaraka hayo ya kutunga Sheria yanafuata utaratibu wa kujadili na kupitisha Miswada ya Sheria inayowasilishwa Bungeni ulioainishwa katika Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, ambazo katika Mwongozo huu zitarejewa kama Kanuni za Kudumu za Bunge.

Kwa upande mwingine, Muswada wa Sheria ukishapitishwa na Bunge unatakiwa kukubaliwa na Rais ambaye amekabidhiwa madaraka na Katiba kwa ajili hiyo. Baada ya hatua hiyo ndipo Muswada unahesabika kuwa Sheria iliyotungwa na Bunge.

Mchakato wa kutunga sheria umewekewa utaratibu na Kanuni ya 80 hadi Kanuni ya 93 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kutokana na mchakato huu kuwa mrefu na wenye kuhusisha masuala mengi ya

utaalamu wa sheria, Sekretarieti ya Bunge imeona umuhimu wa kuandaa Mwongozo utakaomsaidia Mbunge kuweza kuuelewa kwa urahisi mchakato mzima wa kuandaa na kupendekeza Muswada wa Sheria hususan Muswada Binafsi.

Kwa msingi huu, Mwongozo umeandaliwa kwa muundo na lugha rahisi ambayo itamsaidia Mbunge kupata uelewa mpana wa mchakato ambao Muswada Binafsi wa Sheria unapitia kuanzia mwanzo hadi Muswada huo kutungwa kuwa Sheria.

## 2.0 MAANA YA MUSWADA WA SHERIA

Muswada wa Sheria ni mapendekezo ya Sheria mpya au mabadiliko katika Katiba ya nchi au sheria yoyote iliyopo ambayo yanawasilishwa Bungeni kwa ajili ya kuzingatiwa na Bunge ili yaweze kutungwa kuwa sheria. Bunge linapofanyia kazi Muswada wa Sheria linaweza kuujadili, kuuchunguza au kuufanyia marekebisho au mabadiliko. Aidha, Bunge linaweza kuupitisha au kutoupitisha Muswada huo.

## 3.0 AINA ZA MISWADA YA SHERIA

Kuna aina mbili kuu za Miswada ya Sheria ambazo ni, Muswada wa Sheria wa Serikali na Muswada Binafsi wa Sheria. Aina hizi za Miswada zimeainishwa na kufafanuliwa katika Kanuni ya 80 na Kanuni ya 81 ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

(a) **Muswada wa Sheria wa Serikali**

Muswada wa Sheria wa Serikali ni ule unaowasilishwa Bungeni na Waziri, Naibu Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Kanuni ya 82 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ikisomwa pamoja na Ibara ya 55 na Ibara ya 59 ya Katiba.

(b) **Muswada Binafsi wa Sheria**

Muswada wowote wa sheria unaowasilishwa Bungeni na Kamati yoyote ya Kudumu ya Bunge au Mbunge yeyote unaitwa Muswada Binafsi kama ilivyoelezwa katika Kanuni ya 81 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Licha ya kwamba Kanuni hii inatoa fursa kwa Mbunge yeyote kuwasilisha Muswada Binafsi, Mbunge ambaye pia ana madaraka ya Waziri Mkuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri au Naibu Waziri hataweza

kupendekeza Muswada Binafsi wa Sheria Bungeni kutokana na dhana ya mgawanyo wa mamlaka na uwajibikaji wa pamoja.

## 4.0 UTARATIBU KUHUSU MUSWADA BINAFSI WA SHERIA

Mbunge yeyote anayekusudia kupendekeza Muswada wa Sheria anapaswa kuzingatia mambo mbalimbali yaliyowekwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge ili Muswada anaoupendekeza uweze kupitia mchakato wote uliowekwa na hatimaye kuwa Sheria. Mambo hayo yanahusiana na maandalizi ya Muswada pamoja na utaratibu na namna ya uwasilishaji wa Muswada husika Bungeni.

Hata hivyo, iwapo Mbunge atahitaji huduma za usaidizi katika utaratibu na kuandaa na kuwasilisha Muswada Binafsi wa Sheria, huduma hizo zinapatikana kutoka Sekretarieti ya Bunge. Kanuni ya 21 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inaweka utaratibu ambao Kamati yoyote ya Bunge au Mbunge anaweza kuwasilisha masuala ya Sheria (mfano Muswada Binafsi wa Sheria) kwa Katibu wa Bunge na kufanyiwa kazi. Hivyo, Mbunge anaweza kuandaa na kupendekeza Muswada Binafsi yeye mwenyewe

bila msaada wa Sekretarieti au kwa kupata msaada wa kisheria na uandishi kutoka Sekretarieti ya Bunge.

## 5.0 MAANDALIZI YA MUSWADA BINAFSI

Mchakato wa Muswada Binafsi wa Sheria unaanza kwa kutambua eneo la sheria ambalo linahitaji kutungiwa sheria mpya au eneo ambalo lina sheria lakini sheria iliyopo inatakiwa kufanyiwa marekebisho kutokana na sababu mbalimbali kama vile baadhi ya masharti ya sheria husika kupitwa na wakati.

Hatua hii inafuatiwa na utafiti wa kutosha katika eneo husika ambapo inajumuisha, pamoja na mambo mengine:-

(a) Kujua asili au chanzo cha mahitaji ya sheria mpya;
(b) Utafiti wa sheria zinazohusiana na mchakato wa kutunga sheria;
(c) Kutafuta ushauri wa kitaalam;
(d) Utafiti wa sheria za maeneo mengine yanayokaribia kufanana na eneo husika;
(e) Kuzingatia sera, sheria za kimataifa pamoja na mila na desturi; na
(f) Sheria za nchi nyingine zinazofanana na eneo husika.

## 6.0 SHERIA ZINAZOPASWA KUZINGATIWA KATIKA MCHAKATO WA KUTUNGA SHERIA

Sheria zifuatazo ni miongoni mwa sheria mbalimbali za nchi ambazo zinasimamia mchakato wa kutunga sheria hapa nchini.

(a) **Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977**

Katiba ndiyo Sheria mama ya nchi ambayo, pamoja na mambo mengine, inaweka msingi wa madaraka ya Bunge ya kutunga Sheria pale ambapo utekelezaji wa jambo unahitaji kuwepo kwa Sheria.

(b) **Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984**

Kwa kuzingatia muundo wa Muungano wetu, ni vyema kuzingatia Katiba ya Zanzibar kwa kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano lina mamlaka ya kutunga Sheria kwa mambo yote ya Muungano na mambo mengine yote yahusuyo Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa Ibara ya 64 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1977, mamlaka yoyote ya kutunga sheria katika Tanzania Zanzibar juu ya mambo

yote yasiyo mambo ya Muungano yatakuwa mikononi mwa Baraza la Wawakilishi.

(c) **Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016**

Kanuni za Kudumu za Bunge zinafafanua na kuweka utaratibu mahsusi wa namna ya kutekeleza madaraka ya Bunge ya kutunga sheria kama yalivyowekwa na Katiba. Utaratibu huu kwa ujumla umefafanuliwa na Kanuni ya 80 hadi Kanuni ya 93 ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

(d) **Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1**

Sheria hii inaweka majumuisho ya kanuni za msingi zinazohusu maana, ufafanuzi na matumizi ya sheria zilizotungwa, na mambo mengine yanayohusiana na sheria zilizopo pamoja na utungaji wa sheria. Kwa msingi, sheria hii ni ya muhimu katika mchakato wa utungaji wa sheria.

(e) **Sheria ya Mapitio ya Sheria, Sura ya 4**

Sheria ya Mapitio ya Sheria inahusika na maandalizi na uchapaji wa mapitio ya mara kwa mara ya sheria zote pamoja na maboresho

yake. Kifungu cha 7 cha sheria hii kinampa Mwandishi Mkuu wa Sheria mamlaka ya kusahihisha makosa ya kiuandishi au kiuchapaji katika sheria.

Hivyo, sheria hii inaweza kumsaidia Mbunge kujua iwapo sheria fulani inaweza kupendekezewa Muswada wa Marekebisho ya sheria au ni sheria yenye jambo ambalo linaweza kusahihishwa na Mwandishi Mkuu wa Sheria.

(f) **Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296**

Sheria hii inaainisha Kinga, Madaraka na Haki za Wabunge na Bunge kwa ujumla katika kutekeleza madaraka yake. Mojawapo ya haki hizo imewekwa na kifungu cha 3 ambayo ni haki ya kuwa na uhuru wa mawazo Bungeni ambao kimsingi unamwezesha Mbunge kupendekeza Muswada kuhusiana na jambo lolote kwa mujibu wa sheria.

## 7.0 MASHARTI YA JUMLA YA MUSWADA BINAFSI WA SHERIA

Mambo ya jumla ya kuzingatia katika kuwasilisha Muswada Binafsi yameanishwa katika Kanuni ya 81 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Mambo hayo ni:

(a) **Kuandika Muswada Binafsi wa Sheria**

Uandishi wa Muswada Binafsi wa Sheria haujawekewa muundo maalum kisheria. Hata hivyo uzoefu wa utungaji wa sheria mbalimbali hapa nchini unaweka muundo wa jumla wenye mgawanyo katika sehemu mbalimbali ambao sheria zote zinauzingatia.

Masharti ya Muswada ambao sio wa marekebisho ya Sheria iliyopo yatakuwa katika mpangilio ufuatao:-

(i) Jina na tarehe ya kutumika;
(ii) Matumizi;
(iii) Tafsiri;
(iv) Masharti ya msingi;
(v) Makosa na adhabu mbalimbali;
(vi) Masharti ya jumla;
(vii) Masuala ya mpito; na
(viii) Jedwali.

(b) **Kuandaa Taarifa ya Kuwasilisha Muswada Binafsi wa Sheria**

Taarifa ya Muswada Binafsi wa Sheria inapaswa kuwasilishwa kwa Katibu wa Bunge. Taarifa inayowasilishwa kwa Katibu wa Bunge inapaswa kuzingatia masharti yafuatayo ili taarifa hiyo iweze kukubalika:-

(i) Taarifa itaeleza jina la Muswada unaopendekezwa;

(ii) Taarifa itajumuisha madhumuni na sababu za Muswada; na

(iii) Taarifa hiyo inapaswa kusainiwa na Mbunge Binafsi au Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayopendekeza Muswada.

(c) **Muswada kutangazwa kwenye *Gazeti* la Serikali**

Utaratibu wa kutangaza Muswada kwenye Gazeti la Serikali unawekwa na Kanuni ya 81 (3) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 80 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Utaratibu huo ni kama ifuatavyo:-

(i) Muswada wa Sheria kutangazwa na Katibu wa Bunge kwenye Gazeti la Serikali kwa matoleo angalau mawili;

(ii) Kuwe na kitambo cha angalau siku saba tangu kutangazwa kwa toleo la kwanza hadi litakapotangazwa toleo la pili; na

(iii) Taarifa ikitolewa kwenye Gazeti la Serikali inayotaja jina la Muswada, nambari na tarehe ya Gazeti la Serikali ambapo Muswada ulitangazwa mara ya kwanza inatosha kuthibitisha kuwa Muswada umetangazwa kwa mara ya pili.

## (d) Muswada Binafsi wa Sheria wa dharura

Kanuni ya 81 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inaweka utaratibu ambao Muswada Binafsi wa Sheria wa dharura unaweza kuwasilishwa Bungeni. Utaratibu huu hautazingatia masharti ya muda wa utangazaji wa Miswada ya Sheria.

Kwa mujibu wa Kanuni hii, Muswada Binafsi wa Sheria utachukuliwa kuwa ni wa dharura endapo hoja ya kutengua masharti ya muda wa utangazaji wa Muswada itatolewa na kuamuliwa baada ya kuwasilishwa Bungeni hati inayoeleza kuwa Muswada husika ni wa dharura.

Hoja ya kutengua masharti ya muda wa utangazaji wa Muswada Binafsi wa Sheria katika Gazeti la Serikali inapaswa kutimiza masharti yafuatayo ili iweze kukubaliwa kuwasilishwa Bungeni:-

(i) Iwapo ni Muswada wa Kamati, hati hiyo iwe imesainiwa na theluthi mbili ya Wajumbe wote wa Kamati; na

(ii) Iwapo ni Muswada wa Mbunge, hati hiyo iwe imesainiwa na Wabunge wasiopungua kumi.

## 8.0 MAENEO AMBAYO MBUNGE HATAWEZA KUPENDEKEZA MUSWADA BINAFSI WA SHERIA

Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge zinatoa uwanja mpana kwa Mbunge au Kamati ya Kudumu ya Bunge kupendekeza Muswada Binafsi wa Sheria. Hata hivyo, yapo baadhi ya maeneo ambayo yameainishwa na Ibara ya 99 ya Katiba ikisomwa pamoja na Kanuni ya 95 ya Kanuni za Kudumu za Bunge ambayo Mbunge hawezi kuyatolea mapendekezo ya Muswada Binafsi.

Kwa msingi huo, Muswada Binafsi wa Sheria hautashughulikiwa na Bunge iwapo matokeo ya Muswada huo ni mojawapo au zaidi ya kati ya haya yafuatayo:-

(i) Kuweka masharti yanayoanzisha au kuongeza kodi yoyote;

(ii) Kuweka masharti yanayoweza kuongeza kiwango cha fedha zitakazotolewa kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina;

(iii) Kufuta au kusamehe deni lolote linalotakiwa lilipwe kwa Serikali;

(iv) Kubadilisha mishahara au marupurupu ya mtumishi;

(v) Kubadilisha masharti mbalimbali ya utumishi. Masharti hayo ya utumishi ni pamoja na likizo, usafiri au kupandishwa cheo kwa mtumishi yeyote wa Umma; na

(vi) Kufanya mabadiliko katika Sheria, Kanuni au taratibu zinazohusu pensheni, kiinua mgongo au marupurupu mengine ya mtumishi wa Umma au ya mjane, watoto wanaomtegemea au wawakilishi wake.

## 9.0 NAFASI YA SEKRETARIETI YA BUNGE KATIKA UANDAAJI WA MUSWADA BINAFSI

Kwa kuzingatia umuhimu wa shughuli ya utungaji wa sheria, Sekretarieti ya Bunge ina majukumu mbalimbali ikiwemo kuzisaidia Kamati za Bunge na Wabunge kuandika Miswada Binafsi pale itakapohitajika. Majukumu mengine ni kama ifuatavyo:-

(a) Kufanya utafiti wa nyaraka na masuala mengine kadri itakavyohitajika;

(b) Kutoa ushauri kwa Wabunge kuhusu muundo na maudhui ya Muswada;

(c) Kutoa huduma ya uchapaji na uchapishaji wa Muswada Binafsi wa Sheria na nyaraka mbalimbali zinazohusiana nao;

(d) Kutangaza Muswada wa Sheria kwenye Gazeti la Serikali; na

(e) Kufanya uratibu wa shughuli za Kamati ikiwemo kualika wadau kwa ajili ya kutoa maoni.

## 10.0 HATUA ZA MUSWADA KUWASILISHWA BUNGENI

Muswada wowote wa Sheria unapokamilika kwenye hatua za awali hatua inayofuata ni ya uwasilishwaji Bungeni. Kwa mujibu wa Kanuni ya 82 (2) ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge, Muswada Binafsi wa Sheria unapokuwa umekamilisha hatua zote za awali unaweza kuwasilishwa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati yoyote ya Kudumu au Mbunge yeyote ambaye si Waziri. Zifuatazo ni hatua ambazo Muswada Binafsi wa Sheria unapitia unapowasilishwa Bungeni :-

(a) **Muswada Kusomwa Mara ya Kwanza**

Muswada wowote wa Sheria unapowasilishwa Bungeni unapaswa Kusomwa Mara ya Kwanza kwa mujibu wa Kanuni ya 83 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Lengo kuu la Muswada Kusomwa Mara ya Kwanza Bungeni ni kuutambulisha Muswada rasmi katika mchakato wa kibunge. Katika hatua hii, masuala yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa:-

(i) Katibu kusoma jina refu la Muswada husika;

(ii) Hakuna hoja yoyote inayoweza kutolewa kuhusu Muswada huo;

(iii) Hakuna mjadala wowote utakaoruhusiwa Bungeni kuhusu Muswada husika.

(b) **Muswada kupelekwa kwenye Kamati**

Baada ya Muswada wa Sheria Kusomwa Mara ya Kwanza Bungeni, Spika ataupeleka Muswada huo katika Kamati ya Bunge inayohusika kwa kuzingatia maudhui ya Muswada. Kamati itaufanyia kazi Muswada kwa utaratibu ufuatao:-

(i) Kuujadili Muswada mapema iwezekanavyo;

(ii) Kamati itamwalika mtu yeyote afike kwenye Kamati kutoa maoni kwa lengo la kuisaidia katika uchambuzi wa Muswada husika;

(iii) Kamati inaweza kumshauri Mbunge au kushauriwa na Mbunge anayehusika kuhusu kuufanyia mabadiliko Muswada;

(iv) Kamati inaweza kushauriwa na Serikali kuhusu kufanyia mabadiliko au marekebisho ya Muswada Binafsi wa Sheria;

(v) Kamati kuzingatia madhumuni ya mabadiliko au marekebisho yaliyofanyika;

(i) Kamati inapokamilisha kazi yake Mwenyekiti wa Kamati atamjulisha Spika kwa maandishi kwamba, Kamati imemaliza kujadili Muswada husika; na

(ii) Baada ya taarifa hiyo, Spika ataagiza Muswada uwekwe kwenye Orodha ya Shughuli kwa ajili ya Kusomwa Mara ya Pili.

(c) **Muswada Kusomwa Mara ya Pili**

Hatua hii hufuata baada ya Muswada kufanyiwa kazi na Kamati ya Kudumu ya Bunge. Lengo kuu la hatua hii Kikanuni ni kuliwezesha Bunge kujadili kuhusu ubora na misingi ya Muswada wa Sheria.

Mwenyekiti wa Kamati au Mbunge mwenye Muswada husika atawasilisha hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge kuhusu Muswada atakaoutaja kwa jina Kusomwa Mara ya Pili. Katika hatua hii ya kutoa hoja, hakuna hoja itakayotolewa kwa ajili ya kufanya mabadiliko ya hoja ya

Muswada wa Sheria Kusomwa Mara ya Pili inayoweza kuletwa Bungeni isipokuwa kwa mazingira yaliayoanishwa hapa chini:-

(i) Kupendekeza mabadiliko katika hoja bila kutoa sababu. Katika mapendekezo ya aina hii mtoa hoja anaweza kutoa hoja kwamba Muswada husika usisomwe kwa mara ya pili hadi wakati mwingine ambao ni sharti autaje; na

(ii) Kupendekeza mabadiliko katika hoja kwa kutoa sababu ambapo katika pendekezo hili, mtoa hoja ataliomba Bunge likatae Muswada Kusomwa Mara ya Pili kwa sababu atakazoziainisha kwa ukamilifu.

Inapotokea kwamba mojawapo kati ya hoja hizi zimetolewa Bungeni, Spika atalihoji Bunge ili kufikia uamuzi.

Hoja ya Muswada kusomwa Mara ya Pili itafuatiwa na maoni na mapendekezo ya Kamati ya Bunge iliyoufanyia kazi na maoni na mapendekezo ya Serikali. Hatua hii itafuatiwa na mjadala utakaojikita katika

ubora na misingi ya Muswada huo. Katika hatua hii, Mbunge yeyote au Waziri anaweza kumshauri mtoa hoja afanye mabadiliko ya jumla au yale atakayoyataja.

Iwapo mtoa hoja ataona iko haja na kutaka kufanya marekebisho au mabadiliko katika Muswada kutokana na ushauri uliotolewa, masuala yafuatayo yatazingatiwa:-

(i) Mtoa hoja atamjulisha Katibu wa Bunge;

(ii) Katibu wa Bunge atatayarisha Muswada wa Sheria uliochapishwa upya ukiwa na marekebisho au mabadiliko yanayokusudiwa au Jedwali la Marekebisho au mabadiliko yanayokusudiwa; na

(iii) Katibu wa Bunge atagawa kwa kila Mbunge nakala ya Muswada wa Sheria uliochapishwa upya ukiwa na marekebisho au mabadiliko yanayokusudiwa au Jedwali la Marekebisho au mabadiliko yanayokusudiwa.

Vilevile, wakati huu ndio Serikali au Mbunge anayekusudia kufanya mabadiliko katika

Muswada anaweza kuwasilisha mapendekezo yake ya mabadiliko kwa Katibu wa Bunge. Mapendekezo hayo yatakuwa kwenye maandishi yakionyesha bayana kila Ibara inayokusudiwa kufanyiwa mabadiliko.

(d) **Muswada Kufanyiwa Kazi na Kamati ya Bunge Zima**

Mjadala unaofanyika mara baada ya Muswada Kusomwa Mara ya Pili unawaweka Wabunge katika nafasi nzuri zaidi ya kupendekeza mabadiliko au maboresho katika Muswada ambayo yanafanyika wakati wa Kamati ya Bunge Zima. Mabadiliko au maboresho hayo yanapaswa kuzingatia masharti yafuatayo:-

(i) Mabadiliko au maboresho ni sharti yawekwe kwenye Jedwali la Mabadiliko;

(ii) Jedwali hilo la Mabadiliko liwasilishwe kwa Katibu wa Bunge mapema;

(iii) Mabadiliko yakishapendekezwa na kuwekwa kwenye Jedwali la Mabadiliko hayataondolewa isipokuwa kwa idhini ya Spika; na

(iv) Wabunge wote watagawiwa Jedwali

hilo la Mabadiliko;

(v) Mtoa hoja au Mbunge aliyependekeza Jedwali la Mabadiliko anaweza kupendekeza mabadiliko mengine kufanyika katika Jedwali la Mabadiliko alililoliwasilisha mapema kwa kufuata utaratibu wa awali;

(vi) Mabadiliko yatajadiliwa na kupitishwa au kutopitishwa na Kamati ya Bunge Zima kwa mpangilio utakaozingatia mtiririko wa Ibara za Muswada;

(vii) Mtoa hoja ya Muswada Binafsi atapewa fursa ya kwanza kueleza mabadiliko au marekebisho kwa muda wa dakika tano kabla ya Wabunge wengine;

(vii) Mtoa hoja akishahitimisha hoja yake ya mabadiliko, Mwenyekiti ataihoji Kamati ya Bunge Zima ili kupata uamuzi kuhusu hoja hiyo;

(ix) Kwa ujumla, Kamati ya Bunge Zima itajadili na kupitisha au kufanya mabadiliko na kupitisha Ibara moja baada ya nyingine ya Muswada wote wa Sheria;

(x) Baada ya Muswada wa Sheria kupitishwa na Kamati, Bunge litarejea na mtoa hoja atatoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Baada ya hatua hiyo mtoa hoja ataomba kutoa hoja kwamba Muswada husika ukubaliwe na Bunge;na

(xi) Spika atalihoji Bunge kuhusu hoja hiyo kwa ajili ya kufanya uamuzi. Utaratibu wa kufanya uamuzi utategemea na Muswada unaofanyiwa kazi na Bunge kwa wakati husika.

(e) **Muswada Kusomwa Mara ya Tatu**

Hoja ya kuukubali Muswada wa Sheria uliosomwa Mara ya Pili ikishapitishwa na Bunge, Muswada huo utasomwa Mara ya Tatu. Katika hatua hii, Katibu au mtumishi yeyote aliyeidhinishwa kutekeleza kazi ya Katibu atasoma jina refu la Muswada na Muswada utahesabika kuwa umepitishwa na Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 91 ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

## 11.0 MUSWADA KUPATA RIDHAA YA RAIS

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limegawanyika katika sehemu mbili ambazo, ni Rais na Wabunge. Utekelezaji wa majukumu yao katika hatua ya upitishaji wa Muswada unategemeana ambapo kwa kuzingatia Ibara ya 97 (1), Wabunge wanapopitisha Muswada, Muswada huo hautakuwa Sheria hadi utakapopata kibali cha Rais.

Kanuni ya 92 ya Kanuni za Bunge inaweka masharti ya Muswada kupata ridhaa au kibali cha Rais ambapo:-

(a) Katibu wa Bunge atasimamia matayarisho ya Muswada kama ulivyopitishwa na Bunge kwa kuingiza mabadiliko yote yaliyofanyika;
(b) Katibu wa Bunge atatoa nakala mbili za Muswada huo ambapo nakala moja ataiwasilisha kwa Rais kwa ajili ya kupata kibali chake na nakala nyingine ataitoa kwa Spika kwa ajili ya taarifa; na
(c) Baada ya Muswada kukubaliwa na Rais na kuwa Sheria, Katibu wa Bunge atahifadhi nakala halisi ya Sheria hiyo.

Hata hivyo, katika hatua hii Rais anaweza kukataa

kuukubali Muswada. Iwapo Rais atakataa kuukubali Muswada ataurudisha kwa Bunge pamoja na maelezo ya sababu zake za kukataa kuukubali ambapo hatua zitachukuliwa kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 97 ya Katiba. Masharti ya Ibara hiyo yanaeleza kwamba, endapo Bunge litaupeleka tena (mara ya pili) Muswada kwa Rais baada ya miezi sita tangu uliporudishwa na Rais akakataa kusaini Muswada husika ndani ya siku ishirini na moja, Rais atalivunja Bunge.

## 12.0 KUANZA KUTUMIKA KWA SHERIA

Sheria itaanza kutumika tarehe ambayo imetajwa kwenye Sheria husika au kwa Tangazo litakalochapishwa kwenye Gazeti la Serikali. Masharti ya kuanza kutumika kwa Sheria yameanishwa katika Kifungu cha 14 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1.

## 13.0 MATARAJIO KUTOKANA NA MWONGOZO HUU

Mwongozo huu wa Muswada Binafsi wa Sheria kwa Wabunge ni hatua muhimu katika kuimarisha uwezo wa Wabunge kufanya maandalizi muhimu ya Muswada Binafsi wa Sheria. Aidha, Mwongozo

huu utamwezesha Mbunge anayetaka kuwasilisha Muswada Bungeni kufanya hivyo kwa ufanisi kwa kuzingatia Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge. Inatarajiwa kuwa Mwongozo huu utawawezesha Wabunge wenyewe au kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Bunge, kadri Mbunge atakavyoona inafaa, kuanzisha mchakato wa utungaji wa Sheria mbalimbali Bungeni.

## 14.0 HITIMISHO

Inatarajiwa kwamba kupitia Mwongozo huu, uwezo wa Wabunge katika kupendekeza na kuandaa Miswada Binafsi utaongezeka na kuwawezesha kutumia fursa hii adhimu katika kutekeleza madaraka ya Bunge ya kutunga Sheria.

PARLIAMENT OF TANZANIA

UHURU NA UMOJA

BUNGE LA TANZANIA

Mwongozo huu umeandaliwa na
Ofisi yaBunge
S.L.P. 941
Dodoma